**Mambo Ya Kimsingi Kwa**

## MAISHA YA KIKRISTO

# Uwanafunzi 1

## Huduma Ya Uwanafunzi

"Kuufikia Ulimwengu mtu mmoja kwa wakati"

# UWANAFUNZI 1

# Huduma ya uwanafunzi

Kristo, kuwavua, Kujenga na kuwatuma watu kwa ajili ya Kristo!
Huduma ya uwanafunzi ipo kuitimiza tume kuu ya Yesu Kristo mwana wa Mungu ku "Wafanya Mataifa yote kuwa wanafunzi"Kwa kuwavika Kuwafanya wengine kuwa wanafunzi.

The Discipleship Ministry
PO Box 880277
Pukalani, Hawai`i 96788
U.S.A.
e-mail: DiscipleMinistry@aol.com
Website: www.discipleshipministry.com

Mshirikishi -Kenson Kuba

Kenson Kuba ni mhitimu wa Multnomah School of the Bible. Ali hudumu kwenye kamati ya Campus Crusade for Christ kwa Miaka 12 ikiwemo Miaka sita akihudumu kule Papua New Guinea mahali aliishi na mkewe Gail, na watoto wao watatu. kwa sasa anafanya kazi kama mtaalamu wa uchunguzi wa ubora wa maji kwenye Kisiwa cha Maui Hawaii, akiwa na jamii yake, na Mbwa wanne.

* Uwanafunzi 1. Nakiliwa mnamo 1999. Na Huduma ya Uwanafunzi

Maandiko yote yamechukuliwa kutoka kwa Biblia Takatifu ya NIV,isipokua inapo elezwa. Iliyo chapishwa Mnamo mwaka wa 1973,1978,1984 Shirika la Biblia kimataifa ilitumiwa kwa ruhusa ya uchapishaji la Biblia la Zondervan. " Iliyo Chapishwa mnamo Mwaka 1973, 1978, 1984 Jumuhia ya Biblia Kimataifa".

# Yaliyomo


| | |
|---|---|
| **JINSI ya kutumi uwanafunzi** | **3** |
| **1. Hakikisho la Mungu** | **4** |
| **2. Msamaha wa Mungu** | **7** |
| **3. Nguvu za Mungu** | **11** |
| **4. Ushirika** | **15** |
| **5. Neno** | **1** |
| **6. Maombi** | **21** |
| **7. Kushuhudia** | **25** |
| **8. Uzidishaji wa kiroho** | **29** |
| **Agano la Uwanafunzi** | 32 |

## *Jinsi ya kutumia uwanafunzi 1*

### Makusudi

**Uwanafunzi 1** kimetengezwa kuwasaidia wakristo kumtukuza Yesu na kuwavika kuwafanya wengine kuwa wanafunzi!Kinaweza kutumiwa kwa masomo ya kibinafsi,ufuatilizi wa kikristo,uwanafunzi wa mmoja kwa mmoja, uwanafunzi wa kikundi au Seminaa ya mafundisho

### Kukitumia kitabu

**Ufuatilizi & Uwanafunzi**

- Wakristo wapya wanahitajika kufundishwa masomo haya mara hiyo ili kuwapa msingi katika imani yao mpya

- Shiriki masomo kutoka kwenye Uwanafunzi 1na wakristo wengine kuwasaidia wa kue katika imani yao.

- Fundisha na kuwahimiza wale unao jifunza nao washiriki kitabu hiki cha uwanafunzi 1 na watu wengine. Kila mara unapo yashiriki masomo haya na mtu mwengine hautawasadia wao tu katika maisha yao ya kikristo,lakini wewe pia utaendelea kukua unapo pata ufahamu mkuu wa neno la Mungu!

### Muundo
Sehemu kuu kwenye kila ukurasa inahusisha somo hali jedwali upande wa kulia limebeba,maswali,taarifa yenye manufaa,vifungu vinavyo husiana, na maagizo ya kukariri.

### Mkakati
Masomo yaweza kufanywa bila maandalizi ya awali au yaweza kupeanwa na kurejelewa kwenye vipindi vya kujifunza

**SEHEMU KUU ~ Somo**
Soma kwenye masomo yote ukuzingatia nukuu za maandiko yote
Maagizo yanayo ashiriwa na taswira * yakiwemo maagizo kupiga mstari kuweka mviringo au kuisoma sehemu fulani ya maandiko.
Mwanafunzi kuzigundua kweli muhimu kwenye kila somo la Biblia.

**A Kufahamishwa**
Jedwali la kulia. Kwa kila somo
- Umbo linalo akilisha somo,Kwenye jedwali kumsaidia mwanafu azingatie ufahamu wa kina
- Swali la wazo linalo ashiriwa na kishale
- kwenye jedwali humsaidia mwanafunzi
- Inapeana maandiko ya ziada kutazama

Hii inapaswa kuangaliwa kuupata ufahamu bora wa yale maandiko mengine yanafundisha kulihusu somo
A  Mwongozo wa kukariri unao ashiriwa na kishale, inaelzea andiko muhimu la kutafakari.

# 1. Hakikisho la Mungu

## Utangulizi

**Iwapo ungekufa leo unao uhakika gani ya kwamba unao uzima wa milele?** Tia alama kwenye mraba unao angazia jawabu lako.

Sina uhakika, pengine, Hakika kabisa.

Kuna watu wengi ambao wame uthuria kanisa kwa miaka mingi,ambao bado hawana hakika kabi
sa Kuwa na uhakika kuwa unao uzima wa milele inahusisha. **Kweli nne** zifuatazo fafanua uamuzi huu wa muhimu

## Kweli nne

**1. Mungu muumba wetu ana tupenda**

*"Kwa maana jinsi hii Mungu aliupenda Ulimwengu hata akamtoa mwanae pekee, ili kila amwamiye asipotee bali awe na uzima wa milele"*
*Yohana 3:16*

* Weka mviringo kwa neno linalo ieleza nia ya Mungu kutuelekea sisi (Yohana 3:16)
* Piga mstari kwenye fungu linaloeleza jinsi Mungu alivyo uonyesha upendo upendo wake.
* Piga mstari kwenye kile tunapaswa kufanya ili kuupata uzima wa milele.
* Weka mviringo kwa wale uzima wa milele umetolewa.

*"I Mwivi huja ili kuiba na kuua na kuangamiza mimi(Yesu) nimekuja ili wawe na uzima kisha wawe nao tele"*
*Yohana 10:10*

* Piga mstari sababu Yesu anayoisema ameijia 10:10.
* Weka mviringo kwa aina ya uzima anao taka tuwe nao.

**2. Dhambi zetu zimetutenga na Mungu!**

*" Kwa sababu wote wamefanya dhambi,na kupungukiwa na utukufu wa Mungu,"*
*Warumi 3:23*

*"Kwa maana mshahara wa dhambi ni mauti;bali karama ya Mungu ni uzima wa milele katika Yesu kristo Bwana wetu."*
*Warumi 6:23*

* Weka mviringo ni watu wangapi wamefanya dhambi kulingana na Warumi 3:23.
* Piga mstari matokeo ya dhambi kulngana na Warumi 3:23 & 6:23.

**Upendo wa Mungu**
Upendo limetafsiri kutokana na neno la Kiyunani Agape linaloelezea upendo wa kiroho zaidi ya kihisia. upendo wa kihisia mara nyingi ni wa kujitakia,upendo wa Agape hupenda kile kinacho pendwa pasipo kujali gharama kwa yule anaye kipenda.

**Mauti ya kiroho**
Adhabu kwa dhambi zetu ni mauti. Mauti hii ni zaidi ya miili yetu kufa; separation from God Ni utenganao wa kiroho na Mungu. Wakati wa mauti yetu ya kimwili utengano huu unakuwa wa milele.

Huu utengano kati ya mtu mwenye dhambi na Mungu ni mpana sana kiasi kwamba haijali tunaweza kuwa"wema" kiasi gani,hatuna uwezo wa kuliziba pengo,
Kufanya hivyo ingekuwa kama kuogelea kutoka Hawaii mpaka Los Angeles umbali wa maili 2000 juu ya bahari iliyo wazi. Haijalishi mtu ni muogeleaji mzuri kivipi,hata aliye bora atashindwa.

*Warumi 3:10-20*

3. **Yesu Kristo,Mwana wa Mungu,alikufa msalabani kwa ajili ya dhambi zetu!**

*"Yesu akamjibu, "Mimi ndimi njia, na kweli na uzima.Mtu haji kwa Baba,ila kwa njia ya mimi" Yohana 14:6*

* Weka mviringo kwa vitu vitatu ambavyo Yesu anajitajia katika Yohana 14:6.
* Weka mviringo ninani awezaye kumjia Mungu pasipo Kristo.

*"Bali Mungu aonyesha pendo lake yeye mwenyewe kwetu sisi,kwa kuwa Kristo alikufa kwa ajili yetu tulipo ku wa tungali wenye dhambi:" Warumi 5:8*

* Piga mstari jinsi Mungu ame udhihirisha upendo wake kwetu, katika Warumi 5:8.
* Weka mviringo tulikuwa katika hali gani Mungu alipo tupenda.

*"Kwa maana naliwatolea ninyi hapo mwanzo yale niliyo yapokea mimi mwenyewe,yakuwa Kristo alikufa kwa ajili ya dhambi zetu,kama ya nenavyo maandiko,nayakuwa alizikwa, nayakuwa alifufuka siku ya tatu,kama yanenavyo maandiko;Na yakuwa alimtokea Kefa tena na wale thenashara. Baadaye aliwatokea ndugu zaidi ya mia tano pamoja,katika hawa wengi wanaishi mpaka sasa,ila baadhi yao wamelala.Baadaye akamtokea Yakobo; tena na mitume wote,na mwisho wa watu wote alinitokea mimi kama ni mtu aliyezaliwa si kwa wakati wake." 1Wakorintho 15:3-6*

* Piga mstari vitu vinne Kristo alivinya kwa mujibu wa 1Wakorintho 15:3-6.
* Weka mviringo kwa watu Kristo alio tokea akiwa hai baada ya kufufuka toka kwa wafu.

4. **Lazima tumpokee Yesu Kristo kama Mwokozi na Bwana!**

*"Bali wote waliompokea,aliwapa uwezo wa kufanyika watoto wa Mungu" Yohana 1:12*

* Weka mviringo vitu viwili tunavyo hitajika kufanya kufanyika wana wa Mungu (Yohana 1:12)

*"Kwa maana mmeokolewa kwa neema,kwa nia ya imani;ambayo hiyo haikutokana na nafsi zenu, ni kipawa cha Mungu; wala si kwa matendo mtu awaye yote asije akajisifu." Waefeso 2:8-9*

* Weka mviringo jinsi tunavyo okolewa kwa mujibu wa Waefeso Ephesians 2:8-9.
* Piga mstari kwa nini Mungu alichagua kutuokoa kwa njia ya Imani badala ya matendo Waefeso 2:8-9.

## Kumpokea Kristo

Je, wewe kibinafsi umempokea Yesu Kristo kama mwokozi wako na kumtumainia kukusamehe dhambi zako? Kama sivyo,ungependa,je haungependa? omba sala ifuatayo ili kuufanya uamuzi huu wamuhimu sasa hivi!

*"Bwana Yesu mpendwa, ninakiri ya kuwa nimekutenda dhambi na ninahitaji msamaha wako. Ahsante kwa kufa msalabani kwa nafasi yangu msalabani.Nina kupokea maishani mwangu,na kukutumainia wewe tu kama Mwokozi na Mungu. Kwa jina lako nimeomba Amina!"*

**Kariri!**
- Yesu ana maanisha nini anapodai kuwa "njia"? "kweli"? "uzima"?

*Matendo 4:12*
*1 Timotheo 2:5*
*1 Yohana 5:11*

- N' nini cha muhimu kumuhusu Mungu kutupenda hata kabla tumjue na hata kujali habari zake?

**Yesu Kristo ~ Kipawa cha Mungu**
Mungu anamtoa Mwanae,Yesu Kristo, kama malipo ya dhambi zetu.Kristo alipo kufa msalabani, kifo chake Kililipa adhabu ya dhambi zetu.Hii ndio sababu uzima wa milele unapatikana tu kwa njia ya Kristo.

*2 Wakorintho 5:15 & 21*
*Waefeso 1:7*
*1 Petro 3:18*
*Warumi 10:9-10*

- Je, tuna juaje kuwa Kristo alifufuka toka kwa wafu?
- Je, unafikiri watu hawa wote wangekosea?

**Kariri!**
**Kumpokea Kristo**
Neno 'kumpokea Kristo linatumiwa kulieleza tendo la kumuamini Yesu Kristo kama Bwana na Mwokozi, na kuyatumainia yote ameyafanya msalabani kuununua msamaha wetu.

**Kariri!**
- Kwa nini unafikiri Mungu ameuweka uzima wamilele kwenye imani yetu badala ya matendo yetu?

**Muhimu**
*Siyo maneno yaliyo muhumu bali imani yetu. Sharti tumtumainie Kristo kutusamehe dhambi zetu kwani aliahidi kufanya hivyo.*

# Huduma ya Uwanafunzi
## Hakikisho la Uzima wa milele

- Yasome mafungu ya Biblia yafuatayo kisha uyajibu maswali yafuatayo jinsi ya kuwa na hakikika kuwa unao uzima wa milele katika Kristo Yesu.

> *"Na huu ndio ushuhuda:*
> *Mungu ametupatia uzima wa milele,na huu uzima uko katika mwanaye*
> *Aliye na Mwana anao uzima;*
> *asiye na Mwana hana uzima.*
> *Nawaandikia mambo haya ili muamini katika jina la Mwana wa Mungu,ili mpate kujua yakuwa mnao uzima wa milele."*
> *1 Yohana 5:11-13*

* Weka mviringo yale Mungu ametupatia, kulingana na 1 Yohana 5:11-13.
* Piga mstari mahali Uzima wa milele unapatikana.
* Weka mviringo kile mtu anapata iwapo anaye Yesu.
* Weka mviringo kile mtu hana iwapo hajampata Yesu Kristo.
Kulingana na fungu hili je, mtu anaweza kufahamu kwa hakika kwamba anao uzima wa milele?

☐ **Ndiyo** ☐ **La**

* Piga mstari jawabu la fungu hili kwa swali hili.
* Weka mviringo ni akina nani wanaoweza 'kujua' kuwa wanao uzima wa milele.

Je, unaye Kristo maishani mwako? ☐ **Ndiyo** ☐ **La**

Ikiwa 'ndiyo' n' nini kingine ulipokea toka kwa Mungu,?

☐ Uso kamili na mwili wakuambatana.
☐ Utajiri wa Kifetha
☐ Uzima wa milele

## Matumizi

Tuta tamatisha na swali lilo hilo tulilo anza nalo "Iwapo unge kufa leo je, una uhakika ya kuwa unao Uzima wa milele?"

"Ninalo hakikisho kuwa ninao Uzima wa milele,iwapo ninge kufa leo,najua ningekuwa Mbinguni na Mungu."

---

Sahii Tarehe

(Iwapo hauna uhakika kwamba unao Uzima wa milele
soma tena 1Yohana 5:11-13 iliyo juu. Jadili swali lolote unalo weza kuwa nalo na Mchangaji au Muhuduma wako. Ni ya umuhimu kwamba uelewe somo hili maana ndilo msingi wa mengine yote!)

**Kariri!**

**Msingi wa hakikisho letu**

Uzima wa milele hautegemei jinsi tulivyo wema,au jinsi tuavyo hisi. Uko kwenye imani yetu katika Yesu Kristo.Tambua kwamba mafundisho katika 1 Yohana 5:11-13 yameandikiwa "Wale wanao mwamini mwana wa Mungu"!

- Je, 1Yohana John 5:14-15 yahusiana vipi na yale yanafundishwa katika 1Yohan 5:11-13?

*Warumi 1:16-17*

**Hakikisho**
1. Kristo alikufa msalabani kwa ajili yangu.
2. Mungu atanipokea mbinguni nikifa maana ali ahidi hivyo.
3. Ninao uzima wa milele kwa sababu ninaye Kristo!

**A Ombi**
Baba, ninakusifu maana umewaahidi uzima wa milele wote wanao mwami Mwanao Yesu Kristo. Na ahadi zako ni hakika kwani wewe husemi uongo, wala haubadilishi nia, na ninakushukuru kwa hakikisho nililo nalo katika Kristo!Amina

# 2. Msamaha wa Mungu

## UTANGULIZI

**Je, ungekamilishaje usemi ufuatao?**

*Mtu anapo kuwa mkristo, ...*

☐ *Ni dhambi anazo ziungama tu zina samehewa.*
☐ *Dhambi zake zote.Za wakati ulio pita zina samehewa. lakini siza wakati ujao.*
☐ *Anakamilika na hawezi kutenda dhambi tena.*
☐ *Dhambi zetu zote za wakati ulio pita sasa, wakati ujao zina samehewa.*

Tatizo yote yanayo wa kabili wakristo ni dhambi. Katika masomo mawili yafuatayo,hatuta jifunza tu jawabu sahihi kwa neno lililo juu,lakini pia suluhisho la Mungu kuwasaidia wakristo kuzishinda dhami maishani mwao!

## Kukabiliana na dhambi

Somo hili litayajibu maswali manne yatakayo tufundisha jinsi ya kukabiliana na dhambi maishani mwetu:

**1. Dhambi n' nini?**
**2. Ni nani atendaye dhambi?**
**3. Jawabu la Mungu kwa dhambi n' nini?**
**4. Tufanye nini tutendapo dhambi?**

## 1. Dhambi ni nini?

Neno dhambi hulitafsiri neno la Kiyunani linalo maanisha "kuikosa alama". Linaelezea mahali mshale unatua na shabaha iliyokusudiwa. Ona jinsi inavyo tumiwa katika fungu la Biblia lifuatalo.

*"Kwa maana wote wametenda dhanbi na kupungukiwa na utukufu wa Mungu,"*
*Warumi 3:23*

Dhambi 'hamartia (Kyn)
- Kuikosa alama
- Kukosea
- Kutenda kosa

Warumi 3:23 Inaielezea dhambi kama *" kupungukiwa na utukufu wa Mungu".* **Dhambi** ni kushindwa kwa mwanadamu kuishi kwa mujibu wa kiwango kamili cha Mungu. Sote tumeivunja sheria kamili ya Mungu ya kimaadili, katika matendo au mawazo. Hata kushindwa kwetu kutenda kile tujuacho ni chema ni **dhambi**, Hivyo hakuna mmoja kati yetu mkamilfu au asiye na hatia!

**Kariri!**

- Fikiri juu ya mtu mzuri sana unaye jua,je, unaweza kusema mtu huyo ni mkamilifu?
Mbona ndiyo au la?

*Yakobo 2:10*
*Yakobo 4:17*

### Matokeo ya dhambi

*" Nafsi itendayo dhambi ndiyo itakayo kufa."*
*Ezekieli 18:20*

* Weka mviringo kwa neno linalo elezea matokeo ya **dhambi**.
Je, unaamini watu wanaozihalifu sheria za kimaadili wanihitajika kuathibiwa? Hata Mungu pia! Dhambi huleta hukumu ya Mungu ya mauti juu ya wote wenye hatia ya kuzivunja sheria zake kamilifu za kimaadili.

## 2. Ni nani atendaye dhambi?

* Weka mviringo neno katika Warumi 3:23 (Ukurasa ulio tangulia) linaloelezea Mungu humuhesabia mtu yupi kuwa mtenda dhambi.

*"Tukisema kwamba hatuna dhambi, twajidanganya wenyewe wala kweli haimo mwetu, tukisema kuwa hatukutenda dhambi, twamfanya Yeye kuwa mwongo wala neno lake halimo mwetu."*
*1Yohana 1:8,10*

* Piga mstari jinsi 1 Yohana 1:8,10 ina wataja wakristo wanao dai kuwa hawana dhambi au hawajatenda dhambi.

## 3. Suluhisho la Mungu juu ya dhambi n' nini?

* Soma mafungu ya Biblia yanayo elezea suluhisho la Mungu kwa dhambi yaliyo orodhesha pale chini.

*"Na ninyi mlipokuwa mmekufa kwa sababu ya makosa yenu na kutokutahiriwa kwa mwili wenu, aliwafanya hai pamoja naye akiisha kutusamehe makosa yote Akiisha kuifuta ile hati iliyo andikwa ya kutushtaki kwa hukumu zake iliyo kuwa na uadui kwetu,akaiondoa isiwepo tena akaigongomea msalabani."*
*Wakolosai 2:13-14*

*"Basi Yesu akisha kuipokea ile siki, alisema imekwisha akainama kichwa, akaisalimu roho yake."*
*Yohana 19:30*

*"Yeye "Yesu"asiyeijua dhambi alimfanya kuwa dhambi kwa ajili yetu, ili sisi tupate kuwa haki ya Mungu katika yeye."*
*2 Wakorintho 5:21*

In Katika Wakolosai 2:13-14, Mtume Paulo anatumia mfano tokana na mchakato wa kisheria. Katika wakati wake, waalifu walio hukumiwa walipewa "hati ya mashtaka", iliyo orodhesha uhalifu wote waliofanya pamoja na hukumu iliyo hitajika kwa mujibu wa mahakama. Baada ya kukamilisha kifungo, mahakama ilichukuwa ile hati ya", mash taka",nakuweka muhuri wenye maneno haya ya kiyunani "tetelestai", yanayo maanisha imelipiwa kikamilifu. Haya ni maneno haswa, Yesu alitumia katika Yohana 19:30 aliposema, "imekwisha", kabla afe msalabani

* Weka mviringo ni ngapi kati ya dhambi zako zili samehewa kwa mujibu wa Wakolosai 2:13-14.
* Piga mstari juu kile Mungu alifanya na "hati ya mashtaka" iliyo beba orodha ya dhambi zetu na adhabu ya mauti. Kwa "Igongomea msalabani" na Mungu katika hali anamfanya mwanaye Yesu, kulipia dhambi zetu kwa kufa msalabani kwa na fasi yetu. Yesu asinge zilipia dhambi zetu sisi tunge hitajika kfanya hivyo.
* Weka mviringo kwenye neno "imekwisha katika Yohana 19:30.
andika imelipiwa kikamifu juu yake.
* Piga mstari mbona Mungu alifanya hivi kulingana na 2 Wakorintho 5:21.

*Mithali 20:9*
*Muhubiri 7:20*
*Isaya 53:6*
*Isaya 64:6*

- Je, Mungu angeweza kutusamehe pasipo ya kumu dhabihu Mwanaye msalabani, Mbona ndiyo au la?

Kifo cha Yesu Kristo msalabani kili timiza sifa mbili za Mungu. Kili timiza Utakatifu wake, unao hitaji dhambi kuadhibiwa, na kutimiza Upendo Wake ambao unatamani wokovu wa mwanadamu. Kuipitia dhabihu ya Yesu.Mungu anaweza kuuthihirisha upendo Wake kwa mwanadamu, huku akiudumisha utakatifu

**Kariri!**

Wanathiolojia hukielezea kifo cha Yesu msalabani upatanishi kwa niaba ya, maana Yeye ni mwenye kuichukua nafasi yetu akiichukua adhabu ya dhambi zetu Yeye mwenyewe!

## 4. Tunapaswa kufanya nini tufanyapo dhambi?

*"Tukiziungama dhambi zetu (Mungu)ni mwaminifu na mwenye haki kututakasa na udhalimu wote."*
*1Yohana John 1:9*

1Yohana John 1:9 Imeitwa "**Sabuni ya kipande ya wakristo**" Maana imeubeba ufunguu wa kuzishughulikia dhambi maishani mwetu. Kifungu hiki kinaelezea hatua tunayo hitajika kuchukua tufanyapo dhambi.

* Weka mviringo kwenye neno linaloelezea tendo hili.

Neno kuungama linatokana na neno la Kiyuna linalo maanisha kukubali Kukubaliana na Mungu yakuwa tumetenda dhambi! Fahamu pia ya kuwa kifungu hicho pale juu ni neno lenye masharti. Tukiziungama dhambi zetu, Mungu atayafanya mambo mawili kwetu.

* Weka mviringo mambo hayo mawili.

## Matumizi

**1. Omba na kumuuliza Mungu akufunulie dhambi yoyote ambayo hauja ungama kwake.**
**2. Ungama kwa Mungu kwa kukubali ya kwamba umetenda dhambi.Usitoe vijisababu kwa dhambi zako**
**3. Geuka uziache dhambi zako na umuombe Mungu akusaidie kutozitenda tena.**
**4. Dai zile ahadi mbili ambazo Mungu anawapa wale waziungamao dhambi zao kwa mujibu wa 1 Yohana John 1:9.**
**5. Mshukuru Mungu kwa msamaha wake kama kielelezo cha imani yako!**
**6. Kariri 1 Yohana 1:9.**

## Habari njema zaidi!

*"Kisha anaongeza : "Dhambi zao na uasi wao sitaukumbuka tena kabisa."*
*Waebrania 10:17*

*"Kama mashariki ilivyo mbali na magharibi,ndivyo alivyoweka dhambi zetu mbali nasi ." Zaburi 103:12*

*"Haya,njoni, tusemezane,asema Bwana dhambi zenu zijapo kuwa nyekundu sana, zitakuwa nyeupe kama theluji;zijapo kuwa nyekundu kama bendera zita kuwa kama sufu." Isaya 1:18*

**Tafakari!**

*Zaburi 32:5*

Kukiri A homologeo (Kyn)
homo = fanana
logeo = kusema
'Kusema yanayo fanana' au kukubali

- Mbona Mungu ana dai sisi tuziungame dhambi zetu ili tusamehewe?

- Kwa nini ni ya muhimu ku "geuka mbali " na dhambi zetu na sio tu kuziungama?

Mafungu matatu ya Biblia kushoto yanauelezea msamaha wetu katika njia tatu tofauti.
- Tambua Mungu anayajua mambo yote,unafikiri inamaanisha nini, wala hata zikumbuka dhambi? (Waebrania 10:17)
- Mashariki iko umbali gani na magharibi? (Zaburi 103:12)
- Je, Theluji ni nyeupe kiasi gani? (Isaya 1:18)
- Tokana na vifungu hivi,msamaha wetu umekamilika kiasi gani katika Kristo?
- Kariri moja wapo ya vifungu hivi.

## Maswali na majibu

**S: Je, dhambi zangu zote zimesamehewa au zile za kale tu?**
J: Kristo alizifia dhambi zetu zote: wakati ulio pita,sasa na wakati ujao.

*Waebrania 10:8-18*

**S: Ikiwa Mungu amenisamehe dhambi zangu zote,Kwa nini basi nahitajika kuziungama kwake.**
J: Kukiri, kunaturuhusu kuupata msamaha ambao tayari ni wetu katika Kristo Dhambi huuvunja ushirika wetu na Mungu,sio uhusianiano wetu naye.Uhusiano wetu na Mungu kama watoto wake ni kwa mujibu wa upendo wake kwetu usio na masharti, Lakini ushirika wetu Naye unatutegemea sisi kuudumisha utembezi wa ukaribu naye.Wakati dhambi huuvunja huu ukaribu,kuungama huurejesha!

**S: Na je,iwapo bado nina hisi hatia hata baada ya kuungama?**
J: Hatia yoyote inayo salia baada ungamo halisi haitokani na Mungu. Shetani, mshitaki wetu hufurahia kutuweka kwenye safari ya hatia ili kutuzuia kumtumikia Mungu!

*Ayubu 1:1-11*
*Zakaria 3:1*
*Ufunuo 12:9-10*

**S: Je, ni kwanini nina paswa kuziungama dhambi zangu?**
J: Kuziungama dhambi mara kwa mara huuweka ushirika wetu na na Mungu wazi na mpya.Ina uweka moyo kuwa mgumu mbele za Mungu

*Zaburi 66:18*

**S: Na je habari kulipia gharama?**
J: Ikiwa dhambi yako imemuuza mtu fulani,unahitaji kuomba msamaha,kugharimia hasara iwapo inahitajika

*Mathayo 5:23-24*

**S: Je, ninahitatiji kuziungama dhambi zangu mara ngapi?**
J: kama jinsi nilivyo taja pale juu, 1 Yohana 1:9 ni Sabuni ya kipande ya mkristo". Unajiosha kwa Sabuni ya kawaida mara kadha inavyo hitajika, hivyo unahitaji kuungama mara nyingi iwezekanavyo Ungama dhambi zako mara Mungu anavyo kushawishi kuusiana nazo, Hali yoyote ya kuchelewa inampa Shetani nafasi maishani mwetu.

*Waefeso 4:26-27*

# 3. Nguvu za Mungu

## Utangulizi

Je, ungelikalishaje neno hili? Kikolezo muhimu kuishi maisha ya kikristo niku ...

☐ Kuujaza Moyo na maandiko.
☐ Kuomba jinsi uwezavyo.
☐ Kuhuthuria mikutano ya motisha ya kikristo.
☐ Kujihusisha katika huduma.
☐ Kuchagua kutenda yaliyo mema kwa njia ya Mungu.
☐ Hakuna mojawapo kwa hayo.

Kila mojawapo ya chaguo zilizo juu ni ya muhimu kwa kuyaishi maisha ya ki kristo, lakini hakuna inayo hitimu kama iliyo muhimu sana" maana zote haziwezi kushughulikia kizuizi cha kimsingi ambacho wakristo wanapaswa kukishinda, Kizuizi hiki hakiyafanyi maisha ya kikristo kuwa magumu kuishi, bali kuwa isiyo wezekana kuishi! Kwenye somo hili, tutajifunza juu ya upeanaji wa Mungu kulishinda tatizo hili!

## Kwanini hatuwezi kuishi maisha ya kikristo

Kizuizi cha kimsingi kinacho wazuia wakristo ni asili ya dhambi. Kinyume na imani ya kuwa zote huzaliwa bila hatia, Maandiko yanafundisha kuwa hatufanyiki watenda dhambi, bali tunazaliwa watenda dhambi. Chukulia yafuatayo, yaliandikwa na Mfalme Daudi, ambaye Mungu anamuelezea kama

*"Mtu anaye utafuta moyo wangu". Zaburi 51:5*

Tangia wakati tulichukuliwa mimba, tulikuwa tayari tumeharibiwa na dosari la kufisha...hali ya kurithi ambayo inafanya kutenda dhambi sehemu ya asili yetu!
* Soma jinsi maandiko yafuatayo yanalielezea tatizo hili.

*"Hakuna mwenye haki hata mmoja, hakuna anaye fahamu, hakuna amtafutaye Mungu hakuna amtafutaye Mungu. Kila mtu ameigeukia njia yake, wote wamepotoka, hakuna atendaye mema, hakuna hata mmoja." Warumi 3:10-12"*

*"(Yesu alisema) Maana kutoka ndani ya mioyo ya watu, hutoka mawazo mabaya, zinaa, wizi, mauaji, uzinzi, tamaa mbaya, ubaya, uongo, ukaidi, wivu, matukano, majivuno upotovu. Haya yote hutoka ndani ya moyo nakumfanya mtu kuwa najisi'." Marko 7:21-23*

*"Moyo wenye dhambi unamchukia Mungu. Wala haujitiishi chini ya sheria ya Mungu, wala haiwezi kufanya hivyo. Wanao tawaliwa na asili ya dhambi hauwezi kumpendeza Mungu." Warumi 8:7-8*

- Iwapo sisi ni watenda dhambi wakati wakuzaliwa basi unafikiri dhambi yatoka wapi?

*Zaburi 58:3*
*Ayubu 15:14*
*Warumi 5:12*

- Iwapo hakuna amtafutaye Mungu, je, basi mwishoe twampata vipi?

*Yohana 6:65*
*Mathayo 11:27*
*Mathayo 16:17*

Kwa sababu ya asili yetu ya dhambi, haijalishi twayafahamu maandiko mangapi, haijalishi tunaomba mara ngapi, haijalishi tutahuthuria mikutano ya motisha mingapi, haijalishi tunajihusisha katika huduma kivipi,au haijalishi tuna taka kiasi gani kutenda vema, juhudi zetu bora zitashindwa kwa sababu hazishugulikii tatizo kuu! ikifanywa kwa nguvu zetu wenyewe When,kazi hizi haswa huleta kiburi cha kiroho Lakini Mungu amepeana suluhisho kwetu

## Suluhisho la Mungu

Suluhisho la Mungu kwa asili yetu ya dhambi ni , kutupatia Asili mpya! alifanya kwa kumuweka Roho wake Mtakatifu ndani yetu wakati tunampokea Yesu Kristo!
* Yasome maandiko yafuatayo yanayo uelezea muujiza huu.

*"Yesu akamjibu, 'amini nakuambia, mtu hawezi kuuingia ufalme wa Mungu asipo zaliwa kwa maji na Roho.Kilicho zaliwa kwa mwili ni mwili na kicho zaliwa kwa Roho ni Roho.Usistaajabu kwa kuwa nilikuambia hamna budi kuzaliwa mara ya pili.'" Yohana 3:5-7*

*"Hata imekuwa mtu akiwa ndani ya Kristo amekuwa kiumbe kipya, ya kale yamepita, tazama! yamekuwa mapya" 2 Wakorintho 5:17*

*"Na mfanywe upya katika roho za nia zenu; Mkavae utu mpya, ulioumbwa kwa namna ya Mungu, katika haki na utakatifu wa kweli. Basi uvueni uongo mkaseme kwa kila mtu na jirani yake kwa maana tu viungo kila mmoja kiungo na mwenzake. Waefeso 4:23-24*

* Weka mviringo maneno yaliyo kwenye mafungu yaliyo juu yanayo itaja asili yetu mpya. Roho wa Mungu hupachika Asili mpya na nguvu ndani yetu!

*"Nami nitawapa moyo mpya, nami nitatia roho mpya ndani yenu, nami nita toa moyo wa jiwe ulio ndani ya mwili wenu.Nami nitatia Roho yangu ndani yenu, na kuwaendesha katika sharia zangu, nanyi mtazishika hukumu zangu na kuzitenda." Ezekieli 36:26-27*

*"Lakini mtapokea nguvu akisha kuwajilia Roho Mtakatifu; nanyi mtakuwa mashahidi wangu katika Yerusalemu, na katika katika Uyahudi wote na Samaria na hata miisho ya Nchi." Matendo 1:8*

* Weka mviringo vitu vitatu ambavyo Mungu hutupatia katika Ezekieli 36:26-27.
* Piga mstari vitu viwili ambavyo hutokea Mungu anapo muweka Roho wake ndani mwetu.
* Weka mviringo kile tunapokea akisha tujilia Roho Mtakatifu katika in Matendo 1:8.

(Neno "nguvu" hapa la maanisha uwezo wa kuikamilisha kazi) Roho wa Mungu hutupatia shauku (Ezekieli 36:26-27) na nguvu ( Matendo 1:8) ya kuyatenda mapenzi yake!
* Soma Wafilipi 2:13 chini hapa kutoka kwa tafsiri ya The Living Bible.

*"Maana Mungu anatenda kazi ndani yenu, akiwasaidieni kutaka kumtii yeye na pia kuwasaidieni kuyanya yale anayo taka." Wafilipi 2:13 (TLB)*

**Dini dhidi ya Ukristo**
Dini nyingi hufundisha kwamba tunahitaji kufungamana na kiwango fulani cha masharti ya kiroho au sheria ili kuufikilia ukamilifu. Ukristo hufundisha kwamba mwanadamu hana uwezo wa kujibadilisha mwenyewe. Kinachohitajika haswa ni maisha mapya
- Ni maneno yapi katika kila mojawapo ya mafungu ya Biblia, kushoto, yanalielezea wazo hili ?

*Wakolosai 3:10*

- Je, nini muhimu kwa neno Moyo wa jiwe"na " Moyo wa nyama"?

**Roho wa Mungu ndani mwetu**
Shauku ndani mwako ya kumpendeza Mungu ni kazi ya Roho mtakatifu moyoni mwako. Ni ushahidi wa Asili mpya uliyoirithi ulipozaliwa mara ya pili kwa Roho wa Mungu.

**Kariri!**

## Matumizi

**Kuzaliwa kimwili → Kuzaliwa kiroho → Kifo cha kimwili → Umilele**
**Asili ya dhambi → Asili mpya**

Mchoro ulio juu unaonyesha hali yetu kama wakristo. Tunazaliwa Duniani humu tukiwa na **Asili ya dhambi**. Lakini mara tunapo mtumainia Yesu Kristo kuupata msamaha Tunazaliwa "born again mara ya pili" na **Asili mpya** ambayo sio mimi mpya tu, bali mimi halisi, **Asili ya dhambi**, au mimi wa kale kamwe haiwezi kumpendeza Mungu na hata haiki, lakini **Asili yetu mpya** haitamani tu, bali inaweza kumpendeza Mungu kwa nguvu za Roho Mtakatifu.

*Warumi 7:22*
*Wafilipi 2:13*

Tambua ya kuwa Asili ya dhambi ya mkristo itakoma wakati wa mauti, hali Asili yetu mpya itaendelea milele! Changamoto tunazo pata katika maisha haya ni vita kati ya hizi Asili mbili kuyatawala katika mawazo yetu, mioyo yetu na miili yetu. Vipo vitani ndani mwetu. Habari njema ni kwamba mng'ang'ano huu ni wa muda tu (eneo lilo pakwa)! Mara tuko huru tokana na Asili ya dhambi, Asili yetu mpya haitazuiliwa kamwe kuyafanya mapenzi ya Mungu!

*Wagalatia 5:16-17*

- Je, waweza kukumbuka tukio katika maisha yako, wakati Asili yako mpya na Asili ya dhambi zilipigana ndani mwako?

Ni muhimu kuelewa ya kuwa ufunguo kwa ushindi ni **Roho wa Mungu** aliye ndani yetu. Ni kwa kumruhusu Roho wake tu, kuishi kutupitia sisi ndipo tuta yaona mapenzi ya Mungu na nguvu zake! (Tazama Wafilipi 2:13 Kwenye ukurasa wa 12 tena)

* Jifunze waefeso 5:18 pale chini.

# Mkajazwe na Roho

*"Tena msilewe kwa mvinyo ambamo mna ufisadi, bali mkajazwe na Roho."*
*Waefeso 5:18*

**Kariri!**

- Je, kulewa, kunahusishwa vipi na kujazwa na Roho?

Waefeso 5:18 inatufundisha kuutumia upeanaji wa Mungu ili kuishinda dhambi.

* Weka mviringo kile tunahitaji kufanya na Roho.
Mkajazwe" la maanisha kujazwa kikamilifu means to be filled to the full! Mtu aliye A jazwa na Roho" haachi nafasi ya Asili ya dhambi kuyatawala maisha yake! Vifaa vifuatavyo vya kitenzi "Mkajazwe" inatusaidia kuielewa na kuitumia.

**Amri**: Kitenzi hiki chafundisha kwamba tuna "jazwa na Roho kwa tendo la hiari yetu"! Mungu hatuulizi kujazwa na Roho wake iwapo tuna jihisi kufanya hivyo Mungu anatuamuru kujazwa. Haijalishi tuna hisi vipi... haijalishi hali zetu ziko vipi, twaweza kuchagua kujazwa na kumruhusu Mungu kutawala juu ya maisha yetu!

**Kazi ya Mungu**: Kitenzi hiki pia kina ashiria ya kuwa ni Mungu ndiye anaye tujaza. Sisi tunajipeana tu kwake! Tunapo yatoa maisha yetu kwa Mungu, Roho wake hututia nguvu na shauku zake na uwezo!

**Wakati wa sasa**: Mwishoe, kifungu hiki kinatuamuru kuendelea kumruhusu Roho wa Mungu kutujaza ~ Wakati kwa wakati, saa kwa saa, Siku kwa siku, day by day. Hapana ruhusa na hakuna nafasi kwa Asili ya dhambi kutawala!

**Tunawezaje kuwa na hakika ya kuwa Mungu atatujaza na Roho wake?**
Kwa maana ali ahidi atatujaza, na Mungu hadanganyi!

*Tito 1:2*

* Isome ahadi yake katika 1 Yohana 5:14-15.

*"Huu ndio ujasiri tulio nao kwa Mungu: Yakuwa tukiomba kitu chochote kulingana na mapenzi yake, Yeye hutu sikia. Na iwapo twajua kwamba atusikia ~ chochote tuombacho ~ Twajua yakuwa tumepokea kile tumuombacho" 1Yohana 5:14-15*

**Tafakari!**

* Weka mviringo nia tunayo hitaji kuwa nayo tunapo mukaribia Mungu.
* Piga mstari hoja ambazo Mungu husikia.
* Piga mstari matokeo wakati Mungu anayasikia maombi yetu.

*1. Je, ni mapenzi ya Mungu kwetu sisi kujazwa na Roho wake?* □ ndiyo □ la
*2. Tuki muomba Mungu atujaze na Roho, je, atatusikia?* □ ndiyo □ la
*3. Iwapo tunajua Mungu atatusikia, je, twaweza kuwa na hakika tumejazwa?* □ ndiyo □ la

**Kuomba kwa ajili ya mapenzi ya Mungu**

1 Yohana John 5:14-15 inaweza kutumiwa wakati tuombapo chochote kwa mapenzi ya Mungu. Twaweza kuwa na ujasiri yakuwa Mungu atayajibu maombi hayo kwa sababu ali ahidi hivyo.

## Matumizi

Hatua zifuatazo zaweza kutusaidia kuwa na nguvu za Mungu mfululizo:

1. **Kiri** ~ Kuto jazwa na Roho wa Mungu kikamilifu ni dhambi Ungama hili kwa Mungu na udai msamaha wake. (1 Yohana 1:9).
2. **Ukajazwe na Roho mtakatifu** ~ Muulize Mungu akujaze na Roho wake! Mruhusu atawale akilini mwako, moyo na mwili!

## Omba

**"Mungu mpendwa, nisamehe kwa kuiruhusu dhambi kutawala maishani mwangu. Sasa nautoa moyo wangu, akili zangu na mwili wangu kwako na kukuomba unijaze na Roho wako. Nakutaka wewe utawale maishani mwangu! ahsante Mungu kwa kuyasikia na kuyajibu maombi yangu! Kwa jina la Yesu. Amina"**

# 4. Ushirika

## Utangulizi

Mtoto amezaliwa. Miaka kumi baadaye, bado yuko katika kimo na kiwango kama vile alivyo zaliwa! Mwiitikio wako wa mara

☐ "Wau.  Bado mtoto huyu apendeza kweli"
☐ "Sawa ... Nakisia watoto wengine hukua polepole kuwaliko wenzao"
☐ "Mpeleke mtoto huyu kwa Daktari ...Wau!"

Haimuhitaji Daktari kwenye hadidhi yetu kutambua yakuwa mtoto ana kasoro. Watoto wa kawaida hukua na kukomaa, ni kasoro kutofanya hivyo!

Wakati Mungu alimuweka Roho Mtakatifu wake ndani mwako, ulipo muamini Kristo kwa ajili ya msamaha,"**ulizaliwa mara ya pili**" Kiroho. Mara ukafanyika sehemu ya jamii ya Mungu ya milele,"*kiumbe kipya*" katika *Kristo*, umeumbwa kukua kufikia ukomavu, wenye hatima ya kumtukuza Kristo kupitia maisha yako.

*1 Petro 1:23*
*Yohana 1:12*
*2 Wakorintho 5:17*
*2 Wakorintho 6:18*
*1 Petro 2:2*

* Soma 2 Petro 3:18 :

> *"Lakini kueni katika neema na kumjua Bwana wenu na Mwokozi Yesu Kristo. Utukufu una yeye sasa na hata milele! Amina." 2 Petro 3:18*

Masomo manne yafuatayo yata kufundisha kanuni zitakazo kusaidia kuwa na maisha yatakayo endeleza ukuaji wa kiroho katika maisha yako ya kikristo. Kama ilivyo katika ulimwengu wa kawaida, Ukuaji huchukua muda, na kuupata ukomavu wa kiroho unahitaji subira. Lakini uki ya nithamishamisha maisha yako na kuzitumia kanuni hizi, ukuaji wa kiroho yatakuwa ni matokeo yasiyo epukika!

## "Nguvu katika Hesabu!"

Kanuni ya kwanza kuhakikisha ukuwaji wa kiroho ni kuimarisha uhusiano thabiti na wakristo wengine wanao kuwa.

**Kuwa na moto kwa ajili ya Yesu!**

Kama vile makaa huwaka kirefu yakirundikwa pamoja, vivyo hivyo wakristo wanaojiunga na ushirika wa kiroho, watawasha imani ya wenzao katika Mungu, na kuuwasha upendo wa
mmoja na mwingine kwake! Hapa kunazo sababu chache kwa nini tujiunge na ushirika wa kikristo.

# Himizo

*"Tusiache kujumuika pamoja kama vile wafanyavyo wengine, lakini tuhimizane na hata zaidi kama muonavyo siku inakaribia."*
*Waebrania 10:25*

* Piga mstari kile hatupashwi kufanya kulingana na Waebrania 10:25.

* Weka mviringo maneno "*kuacha*". Maneno yana maanisha "*Kuacha kabisa*" au "*Kusahau kabisa*". Wakristo wanakatazwa kuacha kukutana pamoja, Kuacha si chaguo!

* Piga mstari kitendo tunacho hitajika kufanya.

* Weka mviringo neno "**himiza**". Neno hili ni tafsiri ya Kiyunani linalo maanisha Kuita kando kando" Nakuleta taswira nzuri ya mtu akimtia mwenzake moyo, wakiwa wanatembea kando na mwenzake pamoja. Mara nyingi huwa ni rahisi kukosoa, au kuabisha au kumuhuku mwengine asiye fikilia kiwango chetu, lakini Mungu anatuuliza, kuhimiza, kusimama kando kando ya wale wanao yumbayumba.

# Motisha

*"Msidanganyike ushirika m baya huaribu tabia njema.'"*
*1 Wakorintho 15:33*

* Weka mviringo neno linalo elezea kile hatupaswi kufanya (1 Wakorintho 15:33). Neno "**kudanganywa**" lina maanisha kuelekzwa mbali na ukweli, tuna patata onyo kote katika Biblia, pengine kwa sababu tunayo mazoea ya kufikiri tunaijua njia, hata baada ya Mungu kutuambia njia sahihi!

* Weka mviringo kwenye neno linalo elezea madhara ya "*ushirika m baya*" on kwa *"tabia njema"*.
Neno "**kuharibu**" lina maanisha kunajisi au kuangamiza.

Je, ushawai kutana na watu ambao, wakifikiri wange wasaidia watu wengine walio zama katika dhambi, badala yake wamevutwa kwenye dhambi? maisha yamejaa wakristo walio chagu kubaki na ushirika mbaya badaye waipata imani yao imeharibiwa.

*"Msidanganganyike*"! Tutakuwa kama ushirika tunao baki nao, iwapo lengo letu ni kukuwa kiroho na kuwa wakristo walio komaa kiroho, basi lazima tuchukue wakati na wakristo wanao kuwa kiroho hata ukomavu!

**Kariri!**

**"Usi kate tamaa!"**
**Bwana, Winston Churchill**
Muda mfupi baada ya mwisho wa vita vya pili vya Dunia II, Bwana Winston Churchill, ambaye alikuwa ameiongoza Uwingereza kama waziri mkuu, kwenye wakati wake mzuri sana katika vita, alialikwa kuunenea mkutano wenye hari kuu kuyasikia maneno yake ya hekima. Akiwa nasifa za umahiri wake na usemi, umati ulikuwa tayari kwa karamu ya maneno, Waliketi kwa umakini mkuu wakati msemaji boora alipo enda kwenye jukwaa na, kama mpigo wa ngoma, akarudia tena na tena alipo uhimiza umati, "usi wahi kata tamaa"usi wahi kata tamaa, usi wahi kata tamaa, kwa dakika kadhaa, baada ya dakika na rudio la mwisho, aka geuka na kuketi mbele ya umati ulio jaa mshangao.

**Kariri!**

*Mathayo 24:4*
*Mithali 13:20*
*Petro 2:17-22*

- Katika njia gani haswa ndio ushirika mbaya huaribu tabia njema?

- Ni kwa njia gani ushirika mzuri hukuza tabia njema?

## Urejesho

*“Ndugu zangu, mtu akighafilika katika kosa lolote, ninyi mlio wa Roho, mrejezeni upya mtu kama huyo kwa roho ya upole.” Wagalatia 6:1a*

* Weka mviringo kile chaweza kumpata mkristo asiye macho. (Wagalatia 6:1) Neno kughafilika ni kutegwa, kwa mshangao.

